**KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA**

**CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI**

# SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

## MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Mark Finley - Msaidizi wa Mwenyekiti wa Konferensi Kuu.

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

**Juma la Kumi na Nne**

**Juni 26 – Julai 04, 2020**

**TUNAJUA NAMNA KISA KINAVYOMALIZIKA**

Moja ya sababu kuu kwa nini hatuishi katika hofu, tukiwa tumemezwa na wasi wasi na fadhaa ni kwa sababu tunajua namna kisa kinavyomalizika. Tunajua kuwa ugonjwa hautakuwa na kauli ya mwisho: Kristo atakuwa na kauli ya mwisho. Tunajua kuwa kirusi cha Korona, au kirusi kingine cho chote, majanga ya asili, maafa au vita vya nyukilia havitaangamiza uhai wote katika sayari ya dunia. Tunayo ahadi ya kurudi kwa Yesu. Tunaona njaa, Tunaona matetemeko. Tunaona dhiki ya mataifa. Tunaona kuinuka kwa uwezekano wa vita vya nyukilia. Tunaona uwezekano wa janga la nyukilia. Tunaona mabadiliko ya tabia ya nchi. Tunaona tauni zikiangamiza maisha ya maelfu ya watu.

Tunayaona mambo haya, lakini tunalo tumaini linalotuwezesha kustawi katika nyakati ngumu za maisha. Ipo hisia ya ujasiri inayotupitisha salama kwa sababu tumesoma sura za mwisho za Biblia. Tunajua namna kisa kinavyomalizika. Katika Ufunuo 21:4, 5, Yohana anaandika, *"Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, 'Tazama, nayafanya yote kuwa mapya'."* Mtume Paulo naye anasema, *"tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu"* (Tito 2:13).

Sisi ni Waadventista na hatujasahau urithi wetu. Kristo anakuja tena na anakuja upesi. Endapo tutapoteza ndoto yetu ya Kuja kwa Kristo, tutalipoteza tumaini letu. Sisi ni Waadventista. Tunatazama ng'ambo ya hali ilivyo, tunaona hali itakavyokuwa. Tunatazama ng'ambo ya leo, tunaiona kesho. Tunatazama ng'ambo ya ugonjwa, tunaona afya. Tunatazama ng'ambo ya tauni inayosambazwa kwa njia ya hewa, tunaona hewa safi, mahali ambapo hapatakuwa na tauni tena.

Katika majanga ya asili yanayoongezeka, mtikisiko wa kisiasa, ukosefu wa uhakika wa kiuchumi, na tauni kali tunaziona dalili za kuja kwa Bwana wetu. Ingawa Mungu hasababishi haya majanga, anaporuhusu yatokee analo kusudi. Anatuita tumtegemee yeye kwa ujumla na kwa ukamilifu. Anatuita twende kwenye magoti yetu. Anatuita kwenye maisha ya maombi ya kina na uzoefu tele wa kujifunza Biblia. Anatudhihirishia kuwa hakuna uhakika katika ulimwengu tunamoishi. Kristo ni uhakikisho wetu. Yeye ndiye usalama wetu. Yeye ni Mwokozi wetu, Mkombozi wetu, Mwenye kutufungua, Mfalme wetu. Hiki kirusi kinafanya nini tunapokiona kikisambaa kwa kasi? Kinaturudisha kwenye ufahamu.

Ulimwengu huu sio jumla ya yote yaliyopo. Kristo anazungumza kwangu na kwako. Maisha yetu ni dhaifu. Kila mmoja wetu anaishi ndani ya hii miili dhaifu ya udongo. Lakini, ng'ambo ya kilichopo, kuna kitu kingine kilicho bora bado kinakuja – na hicho ni utukufu wa Kristo. Kuna kitu chenye thamani kuishi kwacho, ngambo ya maisha haya na huyo ni Yesu Kristo. Mruhusu aujaze moyo wako, aondolee mbali hofu zako, aimarishe azma yako na kukuandaa kwa ujio wake wa haraka.

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:**
Je! Umetambua ni tumaini gani la ajabu tulilonalo kama waumini wa Kiadventusta? Je! Unaona namna ambavyo hakuna cho chote katika ulimwengu huu kiwezacho kutusukuma chini hasa tunapudumu kuyakaza macho yetu kwa Kristo na ahadi zake? Je! Unapitia kwenye janga hili, na kila siku inakuja, ikiwa na uhakikisho kamili wa ahadi kuu ya Mungu ya shangwe ya milele, furaha na amani?

**CHANGAMOTO ZA MOYONI:**
Tumia muda kidogo leo kutafuta maandiko yote ndani ya Biblia yanayolenga katika tumaini kuu la Kuja Mara ya Pili, na ahadi zinazohusiana na mbingu mpya na nchi mpya. Chagua mafungu machache ili uyakariri, na uruhusu uhalisi wa wema wa Mungu na upendo wake kwako upenyeze ndani ya siku zako tumaini, furaha, na uhakikisho ndani ya Yesu.

*"Na kadiri miaka ya umilele itakavyoendelea, italeta ufunuo tele na wenye utukufu wa Mungu na wa Kristo. Kama maarifa yalivyo endelevu, ndivyo upendo, heshima, na furaha vitatavyokuwa endelevu. Kadiri watu watakavyojifunza zaidi kuhusu Mungu, ndivyo watakavyovutiwa na tabia yake. Yesu anapofungua mbele yao utajiri wa ukombozi na mafanikio ya kushangaza katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo ya waliokombolewa inafurahi kwa ibada ya dhati, na kwa furaha, na kwa shangwe wanapapasa vidubi vya dhahabu; na sauti elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu zinaungana kuikuza kwaya kuu ya sifa. 'Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi, na chini ya nchi, na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele.' Ufunuo 5:13. Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi hawapo tena. Ulimwengu wote ni safi. Pigo mmoja la mwafaka na furaha linadunda katika uumbaji mzima. Kutoka kwake aliyeumba vyote, unatiririka uzima na nuru na furaha, kote katika kingo za anga lisiloweza kuwekewa kikomo. Kutoka kwenye chembe ndogo kabisa ya mada hadi katika ulimwengu mkuu, vitu vyote, vyenye uhai na visivyo na uhai, katika uzuri wao, usio usiofunikwa na cho chote na kwa shangwe kamili, vinatangaza kwamba Mungu ni upendo."* – The Great Controversy, p. 678

**Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:**

- Ellen White, *The Controversy Ended*
- Mark Finley, *Making Friends for God*

**Siku ya 92, Ijumaa, Juni 26, 2020**

**USHUHUDA WA SIFA**

- Divisheni ya Asia Kusini -Pasifiki: Tunamshukuru Mungu kwani kupitia mpango huu zaidi ya mashujaa 5,000 wa maombi wamejiandikisha na kujiunga, wengi wao ni vijana. Mitandao ya maombi imeundwa, na huduma rasmi ya maombi ya vijana imeundwa kwa kupigiwa kura.
- Utoaji kwa Mpango na Huduma za Amana: Tunamshukuru Mungu kwa uaminifu wa Waadventista wa Sabato wakati wa janga la 2020. Tangu Machi 11, 2020 washiriki waaminifu wametoa zaidi ya dola 1,000,000 kwa utoaji wa mpango ambazo zitatumika kusaidia utume wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ulimwenguni kote.
- Tunapokea mamia na mamia ya watu wanaobatizwa kama matokeo ya Siku 100 za Maombi. Tunamsifu Mungu kwa ajili ya kila mtu ambaye amekuwa akiombea mikutano yote ya injili inayoendelea. Utukufu kwa Mungu!
- Mwinjilisti wa Vitabu toka Tanzania: Mungu ametenda muujiza kwangu katika Siku 100 za Maombi. Niliomba Mungu aniunganishe na mtu wa kijifunza naye Biblia. Siku mbili baadaye, mtu mmoja aishiye umbali wa zaidi ya kilomita 7 alikuja nyumbani kwangu. Akasema, 'uliniuzia vitabu, nimevisoma na kugundua ukweli, nimekuja kwako ili niendelee kujifunza' Tunaendelea kujifunza Biblia naye yupo tayari kuyatoa maisha yake kwa Yesu.
- Kijana ambaye sio mwumini wa Kiadventista, aliishi na familia ya Kiadventista wakati wa COVID-19. Familia hiyo ilikuwa ikiomba kila siku, lakini huyo kijana aliwaambia kuwa maombi ni kupoteza muda. Baadaye aliambukizwa corona. Baada ya kusafirishwa hadi mkoa mwingine aliwekwa chini ya karantini. Uzoefu wa karantini ulibadilisha moyo wake akaanza kuwatia moyo wagonjwa wenzake kuomba, kama alivyoishuhudia ile familia ya Kiadventista ikifanya. Matokeo yake, wote walipona kwa muujiza wa Mungu. Yeye na watu wengine 2 wakatoa maisha yao kwa Mungu, na Sabato ya Juni 13 walibatizwa!

**MAMBO YA KUOMBEA:**

- **Mwombee** Lennox. Ni mvulana wa miaka 6. Ana udhaifu wa mfumo wa mishipa mwilini mwake. Lensi za macho yake zimelegea na anaweza kuwa kipofu. Ana umbo la ukubwa usio kawaida, au kijeshi. (yaani, gigantism) na pia moyo wake umetanuka. Ombea watoto wengine wenye magonjwa duniani kote.
- **Ombea** eneo la kaskazini mwa India na maeneo mengine ulimwenguni ambako maambukizi ya COVID-19 yanaongezeka tena.
- **Ombea** watoto wa familia za Kiadventista waliopoteza mwelekeo au wapo katika hali ya kuchanganyikiwa na uasi.
- **Ombea** watu wanaotafakari juu ya kujiunga katika huduma ya injili kwa maisha yao yote. Ombea Mungu awaoneshe wazi wazi wito wao na vikwazo vyo vyote vinavyopaswa kuondolewa.

**Siku ya 93, Jumamosi, Juni 27, 2020**

**NITAKWENDA ... KWENYE FAMILIA YANGU**

*"*Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.*"*– 1 Timotheo 5:8

*". . . inakupasa uwe na bidii, imara, na uliyeazimia kutekeleza majukumu yako katika familia yako, na utembee nayo ikiwezekana. Hakikisha unaweka juhudi zote katika kuwashawishi kuungana nawe katika safari yako ya kwenda mbinguni."* – The Adventist Home, p. 352

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:**

Sote tuna ndugu wa karibu au wanafamilia katika upana wake ambao bado hawajamchagua Yesu na kuamua kuishi kwa uaminifu kwa ajili yake, ama wametanga mbali na Mungu. Inawezekana wengine hawaamini katika Mungu au wanazo sababu zingine katika uamuzi wao. Au huenda hawajawahi kupata nafasi ya kusikia kikamilifu, kuelewa na kuona injili kwa maneno na vitendo. Unao wajibu wa kufanya yale yote yaliyo katika uwezo wako, kuwafikia kwa upole, wema, pamoja na hekima nyingi na upendo, ukiwaonesha kuwa unajali, na katika muda sahihi kuwaonesha ukweli na upendo wa Yesu. Je! Kwa maombi, utaifanya kazi hii muhimu ya upatanisho na kuwahudumia wanafamilia wasioamini/wasio Waadventista/Waliorudi nyuma? Je! Utajitoa na kudhamiria kabisa katika kuwafikia?

**USHUHUDA WA SIFA:**

- Huduma za Familia GC: Katika Siku ya Maombi ya Ndoa na Familia, vikundi visivyo na idadi ulimwenguni kote vilikuwa na mikutano ya maombi usiku mzima ili Mungu aponye ndoa zao na uhusiano wa familia na kulikuwa na miujiza mingi ya ndoa zilizotengemaa na kurejesha amani ndani ya nyumba nyingi zilizokuwa na ugomvi, mivutano, fadhaa na msongo.
- Nancy M.: Mungu aliiponya familia ya binti yangu dhidi ya COVID-19 katika kipindi cha Siku 100 za Maombi na pia ameimarisha mwunganiko wa uhusiano wa familia yangu.
- Nelda M.: Sabato ya Juni 13, tulikuwa na ibada ya kwanza baada ya huduma kurejea tena. Wakati tukiimba wimbo wa kwanza, 'Ikumbuke Kote Sabato ya Bwana,' wengi wetu tulikuwa tukilia machozi ya furaha. Pia tulikuwa na mgeni ambaye hatukumtarajia kutoka mtaa wa jirani ambaye alikuja kuungana nasi. Alisema kuwa analielewa kikamilifu Neno la Mungu kwa kusikiliza tu Redio ya Matumaini. Na yupo tayari kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wake. Tumsifu Mungu!
- Hopewell M.: Katika Siku 100 za Maombi watu zaidi ya 20,000 wamefikiwa kwa njia ya simu na kwa uinjilisti kwa njia ya mtandao na wengi wanasubiri kubatizwa.
- Kiongozi wa kanisa:, Wakati wa zuio la kutotoka nje, kanisa letu lilikuwa na uaminifu na kurudisha zaka kwa asilimia 143 ya goli letu.

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Ombea** ndugu wa karibu wa familia yako na wa mbali. Ombea wokovu wao na fursa za kushiriki pamoja nao imani yako, neno la Mungu, na upendo wa Kristo.
- **Ombea** huduma za vyombo vya habari vya Kiadventista, vihubiri injili ulimwenguni kote bila kuchoka. Ombea mavuno makubwa.
- **Ombea** viongozi wa biashara wanaofanya maamuzi magumu yanayoathiri maisha ya waajiriwa wao wakati wa janga hili.

- **Mwombee** Mathayo, mwanaume anayepambana na uraibu, hana makazi, pamoja na minyororo mingine inayomzuia kupiga hatua kuelekea juu pamoja na Yesu. Ombea apate ushindi yeye na watu wote wa thamani walio chini ya utumwa wa Shetani.

**Siku ya 94, Jumapili, Juni 28, 2020**

## NITAKWENDA … KWA MAJIRANI ZANGU

*"*Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi*."* – Marko 12:31

*"Kazi ya kwanza ya Wakristo ni kuungana katika familia. Kisha, kazi inapaswa ipanuke hadi kwa majirani wa karibu na wa mbali. Wale waliopokea nuru wanatakiwa kuruhusu nuru iangaze kwa miali angavu. Maneno yao yenye manukato ya upendo wa Kristo, yanatakiwa yawe harufu ya uzima iletayo uzima."* – The Adventist Home, p. 37

### MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Yesu anafahamu maeneo yako ya mvuto. Anamjua kila mtu unayekutana naye. Majirani zetu ni maeneo ya utume pia sawa na watu wa nchi za mbali. Tunayo fursa ya kuingiliana nao na kuwa nuru kwao. Lakini hili linataliwa liende mbali zaidi ya tabasamu la kirafiki na maongezi mafupi yanayotokea mara moja moja. Watausikiaje ukweli ikiwa hakuna mtu wa kuwaambia na kuwaonesha? Je! Utaombea kupata fursa za kujenga urafiki na majirani zetu kwa kusudi la kuwashuhudia kuhusu upendo wa Yesu kwao? Kama huwajui majirani zako, upo tayari kuondoka kwenye eneo lako la mazoea na kujitambulisha kwao? Je! Upo tayari kujitoa kwa ajili ya huduma hii muhimu ya uinjilisti kwa majirani?

### USHUHUDA WA SIFA

- Jon R.: Hili janga limeyaleta pamoja makanisa 3 ya mtaa wetu katika maombi kwa njia ya mtandao kila siku katika Siku 100 za maombi. Tunamsifu Mungu, sasa tumeungana zaidi katika moyo na katika utume kuliko wakati mwingine kabla!
- Jackie N.: Ninamsifu Mungu! Tulikuwa wanafamilia zaidi ya 20 katika nyumba moja wakati wa zuio la kutotoka nje, lakini naweza kushuhudia kuwa hatukupata uhaba wa chakula na hakuna aliyeugua!
- Aldo N.: Wakati wa Siku 100 za Maombi nilijifunza kuomba kwa unyenyekevu. Matokeo yake Mungu alitubariki, na mke wangu aliyekuwa hawezi kutunga mimba, na sasa ana mimba!
- N.J.: Mimi na mama yangu tulikuwa tukiomba kila siku saa 11 asubuhi na saa 6 usiku kwa ajili ya baba yangu mwenye miaka 88 ili wapatane na dada yangu. Mungu asifiwe kwani hawa wawili walitembeleana na upatanisho unaendelea!
- Niliweza kuwahudumia majirani zangu kwa kuwapatia vipeperushi vyenye kanuni za Mungu za afya. Mungu alinisaidia kuondoka kwenye eneo langu la mazoea na sasa nina mwunganiko na watu walio katika ujirani na mimi!

### MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** majirani zako, na ujirani wako. Ombea Mungu akuunganishe, akusaidie na kukufanya ujenge urafiki na majirani zako ili uweze kuangaza nuru ya Yesu katika maisha yao.
- **Ombea** kituo kiitwacho, ReNewed Hope Food Pantry, kilichoko Overland Park, Kansas, Marekani. Kinagawa chakula, kinawatia watu moyo, na matumaini, kikizifikia zaidi ya familia 600 (watu kati ya 2500 - 3000) kila juma na kimegawa zaidi ya Masomo 2,000 ya Biblia na vitabu vya Njia Salama vya Kiingereza na Kihispania. Ombea huduma zote za kituo hiki kwa ajili ya ushuhudiaji duniani kote.

- **Ombea** watu wote waliojiunga na huduma kwa njia ya mtandao kupitia mitandao ya kijamii, video, programu tumishi (Apps) na tovuti za kujifunza Biblia. Ombea mavuno makubwa!
- **Ombea** ndoa zilizo kwenye ukingo wa talaka. Mwombe Mungu aponye mahusiano, omba kwa ajili ya msamaha, na upendo kama wa Kristo uweze kuamka

**Siku ya 95, Jumatatu, juni 29, 2020**

## NITAKWENDA … KWA MARAFIKI ZANGU

*"*Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.*"* – Yohana 15:13

*"Kila mshiriki wa kanisa anatakiwa kujisikia ni jukumu lake maalumu kuwafanyia kazi wale wanaoishi jirani naye. Inakupasa kujifunza namna unavyoweza kuwasaidia vema wale wasiopendelea mambo ya kidini. Unapowatembelea marafiki zako na majirani, oneshakuwa unayapenda mafanikio yao ya kiroho na ya muda mfupi. Muwasilishe Kristo kama Mwokozi mwenye kusamehe dhambi. Waalike majirani zako nyumbani kwako, na usome pamoja nao kutoka kwenye Biblia ya thamani na vitabu vinavyoelezea ukweli wake. Jambo hili, likiungana na nyimbo na maombi ya dhati, litagusa mioyo yao. Hebu washiriki wa kanisa wajielimishe katika kuifanya kazi hii. Hii ni muhimu kama ilivyo muhimu kuokoa roho zilizo gizani katika nchi za kigeni. Wakati wengine wakihisi mzigo wa roho zilizo mbali, hebu wale wengi walioko nyumbani wahisi mzigo wa roho za thamani zinazowazunguka na wafanye kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wao"* – Testimonies, Vol. 6, p. 276

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Yesu anatuchukulia mimi na wewe kama marafiki zake. Ni wazo zuri kiasi gani! Alikuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili ya wokovu wetu, alifanya hivyo hata kama ukubali wetu wa kuipokea zawadi yake ulikuwa haujahakikishwa. Je! Unao marafiki wasiomjua Yesu bado? Labda, umekuwa mwoga kumshuhudia Kristo kwa hofu ya kupoteza urafiki wenu? Ikiwa Yesu alikuwa tayari kuutoa uhai wake, ndio, kila vile alivyo, kwa ajili ya wokovu wa rafiki zake, haingetupasa sisi kufanya yote tuwezayo kuwatia moyo marafiki katika njia ya kutembea kwa uaminifu na Yesu? Mwombe Mungu katika maombi namna ya kufanya uinjilisti kwa marafiki. Mwombe akupatie fursa kushuhudia juu ya imani yako, upendo wa Yesu, na namna wanavyoweza kupata uzoefu wa neema ya Mungu inayookoa pia!

**SHUHUDA ZA SIFA**

- Mtu ambaye hajatajwa jina: Janga la kirusi cha Corona limetufungua macho yetu kuhusu ukaribu wa kuja kwa Yesu. Tunamshukuru Mumgu kwa ajili ya Siku 100 za Maombi. Sasa tunaomba zaidi kama familia. Siku moja katika Mwezi wa Mei tulipata ajali mbaya sana ambayo ingeweza kusababisha majeruahi, lakini tunamsifu Mungu tuliondoka bila hata mchubuko mmoja! Siku ile katika safari yetu tulikuwa tumeomba mara mbili. Mungu ni mwaminifu!

- Ruth A.: Nilimwomba Mungu anipatie fursa ya kumshuhudia jirani yangu na alinifungulia mlango ili nimshuhudie Kristo. Jirani yangu ni mgonjwa na alianza kumwamini Mungu!
- Ofisi ya Divisheni ya Kusini mwa Pasifiki: Maombi mawili mahususi kwa ajili ya wagonjwa wa COVID-19 yalijibiwa kwa namna iliyo chanya. Watu wote wawili walikuwa mahututi na ni muujiza tu uliokuwa unatarajiwa kuwarudisha. Wote wawili walipona!

- Alicia S.: Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya Siku 100 za Maombi, kwa sababu katika siku hizi, Mungu amenifunulia dahambi zangu nilizokuwa sijaungama, moja ikiwa ni ubinafsi, yaani kulenga tu kwenye matatizo yangu. Kuomba kila siku kwa ajili ya wengine kunakuza ndani yangu moyo wa upendo unaojali.

- Lo R.: Nimekuwa nikiomba kwa bidii ili nipate mtu nitakayeshiriki naye habari za Yesu. Niliomba kwamba atokee mtu fulani aniombe kwa dhati. Leo nilitembelea biashara moja na huyo mwanamke aliniomba endapo nina vipeperushi niweze kumpatia. Nilimwambia kuwa ninavyo tani nyingi. Nilimpatia *Steps to Christ* (yaani Njia Salama), nikachukua namba yake ya simu na nina matumaini juu ya mengi zaidi. Hii ni mara yangu ya kwanza kumtumainia Mungu kwa namna hii.

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Waombee** marafiki wasioamini. Omba kwa ajili ya hekima ya kushiriki nao injili katika muda sahihi.
- **Ombea** wale wenye chamngamoto ya afya ya akili, wanaojihisi wametengwa, wana wasiwasi, na hawana msaada.
- **Ombea** kanisa kule Toronto, Kanada, kwa namna ya pekee limejipanga kuwahudumia wenye shida, linatoa mahali pazuri kwa ajili ya kuabudia na kujenga urafiki.
- Ombe viongozi wote wa kanisa, wachungaji, na Konferensi, unioni, divisheni na viongozi wa Konferensi Kuu na wafanya kazi. Mwombe Mungu awapatie hekima ili waweze kuyahudumia maeneo yao vema.

**Siku ya 96, Jumanne, Juni 30, 2020**

**NITAKWENDA … KWA WAFANYAKAZI WENZANGU**

*"*Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni*."* – Matthayo 5:16

*"Kutokana na nuru ambayo Mungu amenipatia, ninajua kuwa kazi yake leo ipo katika uhitaji mkubwa wa wawakilishi hai wa ukweli wa Biblia. Wachungaji waliowekewa mikono pekee yao hawatoshi katika jukumu. Mungu hawaiti tu wachungaji, lakini pia waganga, wauguzi, wainjilisti wa vitabu, watendakazi wa Biblia, na walei wengine waliojitoa wakfu, wenye talanta mbali mbali, wanaoujua ukweli wa leo, kuyafikiria mahitaji ya miji ambayo haijapewa onyo. Wanatakiwa wawepo waumini mia moja wanaofanya kazi ya utume mahsusi mahali ambapo kwa sasa yuko mmoja tu. Wakati unapita haraka. Kuna kazi bado zinazotakiwa kufanyika kabla upinzani wa kishetani haujafunga njia. Kila uwakala ni lazima uwekwe kazini, ili fursa za sasa ziweze kuboreshwa kwa hekima."*– Ministry to the Cities, p. 108

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Kila wakati unapokwenda kazini unaingia kwenye shamba lako la utume. Mungu alijua kuwa utakuwa pale kabla hujazaliwa, na kama utamruhusu, atatenda kupitia kwako ili kuwaongoza wafanyakazi wenzako chini ya msalaba. Je! Utamwuliza Yesu, kuwa ni nani unayetakiwa kumshuhudia mahali pako pa kazi? Utaanza kuwaombea wafanya kazi wenzako kwa majina na kumwomba Mungu akupatie fursa za kumshuhudia Kristo?

**USHUHUDA WA SIFA**

- Divisheni ya Inter-America: Nchini Guatemala, mshiriki wa kanisa alianzisha mpango wa kujifunza Biblia kwa njia ya mtandao; masomo hayo yalipelekea Hakimu Mkazi wa Makama Kuu ya Quetzaltenango kubatizwa. Matokeo mikutano ya injili kwa njia ya mtandao katika Unioni ya Kusini mwa Venezuela yalikuwa ni ubatizo wa watu 396 ikijumuisha wachungaji na washiriki wa madhehebu mengine!
- Tumepokea taarifa zisizo na idadi za makanisa, familia, wenzi wa ndoa, na watu binafsi waliojipatia uamsho binafsi, uponyaji, fursa za utume, na baraka ya pekee ya Mungu katika Siku 100 za Maombi. Taarifa ni nyingi mno haiwezekani kuziorodhesha hapa!
- Beverly T.: Tutaendelea kuomba kama kikundi hata baada ya Siku 100 za Maombi!
- Marlene M.: Dada yangu na mume wake wanafanya kazi katika meli na walikwama mle kwa majuma mengi. Nilikuwa nikiomba na kufunga kwa ajili yake. Nilikuwa naweza kushiriki Maandiko pamoja naye katika kipindi hiki cha kutisha, na yeye pia alifuatilia mikutano ya injili iitwayo, 'Hope Awakens' iliyofanywa na Redio ya Waadventista Ulimwenguni (AWR) kwa njia ya mtandao. Aliamua kubatizwa!
- Lillian K.: Tangu zilipoanza Siku 100 za Maombi lilikuwa natumia muda wangu kwa maombi badala ya kula chakula kazini. Matokeo yake nilipitia uponyaji na saumu yangu umekuwa ni wakati maalumu kukaa miguuni pa Yesu.

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Waombee** wafanyakazi wenzako. Omba kwamba maisha yako, maneno, na matendo yawe ushuhuda wa uwepo wa Yesu ndani ya moyo wako. Mwombe Mungu akuoneshe wafanyakazi wenzako waliotayari kujifunza zaidi kuhusu Mungu.
- **Ombea** huduma saidizi za Kanisa la Waadventista wa Sabato. Omba Mungu abariki juhudi zao katika kuendeleza kazi ya kusambaza injili. Ombea hekima ya viongozi na wafanyakazi wao, na Mungu awapatie mahitaji yote ya huduma.
- Ombea Sesheni ya 2021 ya Konferensi Kuu. Ombea mwelekeo sahihi na endelevu kwa ajili ya utume wa Kanisa la Waadventista wa Sabato. Omba kwamba uchaguzi wote na uteuzi wa viongozi kupitia Sesheni ya GC mwezi Mei 2021, na mwaka mzima wa 2021, uwe kadiri ya mapenzi Bwana kwa ajili ya kumaliza kazi duniani kwa nguvu na ujio wake upesi.
- Omba kwa jili ya familia zilizotenganishwa, na watu waliokwama katika nchi za kigeni kutokana na janga hili na mazuio yake. Waombee ili waweze kuutumia huu wakati wenye changamoto kuangaza nuru ya Kristo mahali walipo.

**Siku ya 97, Jumatano, Julai 01, 2020**

**NITAKWENDA … KWA WALE NILIOSOMA NAO**

*"*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia . . .*"*– Warumi 1:16

*"Chukua dini yako hadi katika maisha yako ya shule, ndani ya bweni lako, na katika harakati zako zote."* – Messages to Young People, p. 36

*(Shetani) anajua vema kuwa hakuna daraja linaloweza kufanya mema mengi kama la vijana wa kiume na vijana wa kike waliojiweka wakfu kwa Mungu. Vijana, ikiwa wako sawa, huwa na mvuto wenye nguvu. Mvuto walionao wahubiri, au walei wenye miaka mingi kwa vijana, haufikii hata nusu ya ule walionao vijana, waliojitoa kwa Mungu, juu ya washirika wao. Inawapasa kujisikia kuwa wajibu umewekwa juu yao kufanya yote wanayoweza ili kuwaokoa wenzao wenye kupatikana na mauti kama wao, ikibidi, ni lazima wajiweke wakfu kwa Mungu."* – Messages to Young People, p. 204

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Ikiwa wewe ni mzazi, unaitwa kumsaidia mtoto wako katika kumwonesha namna ya kupenda kama Yesu, na namna ya kushiriki injili na wengine. Je! Utachagua leo kuwa mmishonari kwa watu wa shuleni kwako, kuwa balozi wa Yesu kwa wanafunzi wenzako wa zamani/wa sasa na wa wakati ujao?

Je! Upo shuleni? Una rafiki unaosoma nao darasa moja, wanafunzi wenzako walio katika kutafuta shahada na elimu bora? Unatambua kuwa unachotakuwa kuwapatia – injili – ni ya thamani zaidi kuliko shahada au elimu unayoweza kuitoa ulimwengu huu? Wala unaosoma nao, wanajua kuwa wewe ni Mkristo, Mwadventista wa Sabato? Ama ulihitimu chuo muda mrefu uliopita. Je! Bado unayo mawasiliano au urafiki na wale uliosoma nao?

Mungu anakuita, iwe ni mwanafunzi katika mazingira ya Kikristo au shule ya umma, ili uwe nuru kwa wale unaosoma nao. Iwe unawasiliana nao kwa njia ya simu, mtandao (kwa sababu ya janga) au ana kwa ana, angaza nuru ya Yesu!

**USHUHUDA WA SIFA**

- Sifa kwa Mungu kwa kutupatia miujiza isiyohesabika ya kifedha, kazi, na msaada kwa watu wengi wakati wa zahama hii.
- Joel B.: Mimi na mke wangu tuliwatembelea watoto wetu katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Kwa sababu ya hili janga tulikwama kule na wote tuliambukizwa COVID-19. Maombi mengi yaliombwa kwa niaba yetu. Sisi wote, isipokuwa mke wangu tulipona. Bado ninamshukuru Mungu kwa uongozi wake. Anajua kilicho bora kwa ajili ya familia yetu.
- M.A.: Mnano Juni 9, niliamka saa 8:00 usiku, nikiwa mbele ya mwanaume mwenye bunduki aliyesimama kwenye chumba changu ambamo mimi na watoto wangu tulikuwa tumelala. Alitishia kuua watoto wangu. Tuliogopa, lakini nilimwambia, "Katika jina la Yesu, Ondoka!" Mungu alisikia kilio changu, yule mtu aliondoka bila kutufanyia madhara. Mungu ni mwaminifu!

- Lindinkosi N.: Jioni ya Siku ya 80 (Uponyaji wa Kimwili), uhai wa kaka yangu ulikaribia kutoweka mbele ya macho yetu. Shinikizo lake la damu lilikuwa juu, na mapigo yake ya moyo yalikwenda kasi. Alikuwa anatetemeka, akihangaika kuvuta hewa na hali yake iliendelea kuwa mbaya kila dakika. Kwa haraka tukampatia punje ya kitungu saumu na nusu kijiko kidogo cha pilipili aina ya cayene iliyoyeyushwa kwenye maji. Kisha tulipiga magoti na kuomba, na tulipokuwa tunamaliza kuomba, shinikizo lake la damu likarudi kuwa la kawaida, alitulia kutetemeka na mapigo yake ya moyo hayakwenda mbio tena. Tulimshuhudia Mungu akitenda muujiza wa uponyaji wa kimwili ndani ya dakika 10!

- Rodel L.: Wakati tulipozuiwa ndani, mke wangu alifikiria kuanzisha programu ya kugawa chakula kwa wenye mahitaji. Tulipanga kuanza na vifurushi 30, lakini Mungu alitoa na kuzidisha chakula chetu na vifurushi, akatuwezesha kuzisaidia familia zenye mahitaji kutoka kanisani kwetu na jamii hata kwa miezi inayokuja. Sifa zote zimwendee Mungu wetu wa ajabu!

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Ombea** shule yako, walimu, na wanafunzi unaosoma nao. Ombea ujasiri wa kusimama kama Mkristo anayeishi kwa ajili ya Yesu. Ombea fursa za kuitambulisha imani yako kwa wanafunzi wenzako. Ikiwa haupo shuleni tena, ombea njia za kuwafikia wanafunzi wenzako wa zamani.
- **Ombea** huduma za malezi ya kiroho kwa wanafunzi wa vyuo vikuu inayofanyika kwenye vyuo vya umma ulimwenguni kote. Ombea baadhi ya wanafunzi Waadventista wa Sabato na walimu ili waingie kwenye huduma hii, ya kuufikia ulimwengu kwa kuwafikia wanavyuo.
- **Ombea** mavuno makubwa ya roho kutokana na huduma zote zilizokuwa zikifanyika, kuwafikia watu kwa njia ya mtandao kwa sababu ya janga hili.
- **Ombea** dada zetu wajawazito ulimwenguni kote ambao hivi karibuni watazaa watoto. Waombee wapate usalama na ulinzi dhidi ya COVID-19, na watoto wao watakaozaliwa wawe na afya njema. Ombea watoto hao wakue hadi kuja kuwa watendakazi wa Yesu.

**Siku ya 98, Alhamisi, Julai 02, 2020**

**NITAKWENDA … KWENYE MJI WANGU**

*"*Kautakieni amani mji ule, ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa Bwana; kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani . . .*"*– Yeremia 29:7

*"Umuhimu wa kupenya katika miji mikubwa bado upo mbele yangu. Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akituhimiza kuhusu wajibu huu, na bado tunaona ulinganifu mdogo wa kilichofanyika kwenye vitongoji vikubwa vyenye watu wengi. Ikiwa hatuichukulii kazi hii kwa umakini mkubwa, Shetani ataongeza magumu ambayo haitakuwa rahisi kuyavuka. Tupo nyuma sana katika kufanya kazi ambayo ilitakiwa tuwe tumeifanya katika hii miji iliyoachwa kwa muda mrefu. Sasa kazi itakuwa ngumu zaidi kuliko ambavyo ilikuwa miaka michache iliyopita. Lakini kama tukiichukua katika jina la Bwana, vikwazo vitavunjika, na ushindi mkubwa utakuwa wetu ."* – Ministry to the Cities, p. 25

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Watu walio wengi ulimwenguni wanaishi mijini. Wakati inatupasa kumwomba Mungu atuoneshe ni lini twende mashambani, haitupasi kupuuza kazi ya Mungu katika miji. Mabilioni ya watu wamenaswa katika uraibu pasipo tumaini, makeleke, bughudha, mtindo wa maisha ya mijini. Mwombe Mungu akupatie mzigo kwa ajili ya huduma katika miji. Yawezekana anakuita kuanzisha "kituo cha mvuto," biashara yenye sura ya huduma, ili kuzifikia roho zilizopotea katika miji ya ulimwengu? Au yawezekana anakuita wewe na kanisa lako kuanza mpango wa kuwafikia watu kupitia huduma mbali mbali katika mji wako. Kwa nini usimwombe Mungu akuoneshe namna bora ya kuwahudumia watu wa mji wako?

**USHUHUDA WA SIFA**

- Grant L.: Ili kufidia siku za shule zilizopotea serikali ya Afrika ya Kusini imeongeza juma la masomo hadi siku 6, zikijumuishwa Jumamosi. Unioni ya Afrika ya Kusini ilikata rufaa serikalini ili wanafunzi Waadventista wa Sabato, waruhusiwe kutohudhuria madarasani siku za Sabato na serikali ilikubaliana na rufaa hiyo. Tunamsifu Mungu kwa kuyasikia maombi yetu!
- Dalma O.: Sifa zimwendee Mungu Mwenye nguvu kwani ni mwaminifu kwa ahadi zake. Ninafanya kazi kama Mwinjilisti wa Vitabu nchini Kenya. Nimepata baraka za Mungu wakati wa hili janga. Nilitambua kuwa mauzo yameongezeka mwezi wa Machi, mtiririko ni thabiti!
- Amanda A.: Ninawasiliana na askari wa Marekani katika ukanda wa vita. Ninashiriki nao Siku 100 za Maombi na ninaweza kona Mungu akifanya kazi ndani ya mioyo yao na kwa maamuzi wanayofanya vitani.

- Mtu ambaye hakutajwa jina: Tangu zamani kadiri ninavyokumbuka, baba yangu alikuwa mlevi wa pombe. Kama familia tumekuwa tukiomba ili Mungu amfungulie toka katika utumwa huo, na kwa hakika ametenda! Baba yangu pia anashiriki katika vipindi vya Siku 100 za Maombi na tena ana shauku ya kuongoza vipindi vya maombi!

- Tulipokea taarifa kutoka kwa watoto wanaoshiriki kwa bidii katika mikutano ya maombi ulimwenguni kote! Tumsifu Mungu, Roho wake anafanya kazi kupitia watoto!

**MAMBO AYA KUOMBEA**

- **Ombea** nchi yako na miji ya ulimwengu ambayo inazidi kugeuka na kuwa Sodoma na Gomora. Mwombe Mungu akusaidie wewe, familia yako, na kanisa lako katika kuanzisha vituo vya mvuto, huduma na njia mbali mbali za kuwafikia mabilioni ya watu wanaotanga gizani katika miji.

- **Ombea** duka la vyakula bora nchini Latvia lililofunguliwa na Injinia kijana, ambaye aliacha kazi yake ili afanye kazi kwa muda wote katika kile anachokiita "uinjilisti wa biashara." Tafadhali mwombe Mungu aibariki biashara hii, afungue mwunganiko na jamii, na kuwasaidia wateja wapate njaa ya chakula kitakachowaletea uzima wa milele. Ombea vituo vyote vya mvuto ulimwenguni kote, na Waadventista wengi zaidi wanaoanzisha biashara zinazolenga utume.

- **Ombea** baa ya sharubati (juice bar), Ogaden, Utah inayowafikia vijana. Tafadhali omba kwa ajili ya mafanikio na ili huduma hii iweze kuigwa katika maeneo mbali mbali ulimwenguni kote.

- **Ombea** kituo kiitwacho "Vibrant Life Medical and Wellness Clinic" kule Bangalore, India, ambacho kinatoa huduma za tiba za asili kwa magonjwa sugu kama vile ugonjwa wa moyo, unene kupita kiasi, na kisukari. Tafadhari mwombe Mungu amwage Roho wake kwa wafanyakazi ili upendo wake utiririke kupitia kwao hadi kwa watu wanaowahudumia.

**Siku ya 99, Ijumaa, Julai 03, 2020**

**NITAKWENDA … KWENYE ULIMWENGU WANGU**

*"*Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa.*"* – Ufunuo14:6

*"Mungu, kwa mkono mmoja anakupatia imani, ushikilie mkono wake wenye nguvu, na kwa mkono mwingine anakupa upendo, zifikie roho zinazoangamia. Kristo ndiye njia, kweli, na uzima. Mfuate. Usiufuatishe mwili, bali ifuate Roho. Tembea kama yeye alivyotembea. Haya ni mapenzi ya Mungu, yaani kutakaswa kwenu. Kazi unayotakiwa kuitimiza ni kufanya mapenzi yake yeye anayetegemeza maisha yako kwa ajili ya utukufu wake. Ikiwa unaifanya kwa ajili yako mwenyewe, haitakufaidisha kwa lo lote. Kufanya kazi kwa ajili ya manufaa ya wengine, kujijali kidogo na kutoa yote kwa Mungu kwa bidii, kutakubalika naye na kurudishiwa kwa neema tele."* – Testimonies, Vol. 2, p. 170

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Waadventista wa Sabato wana wito maalumu, wito wa kiunabii wa kutangaza Ujumbe wa Malaika Watatu kwa ulimwengu wote kwa ajili ya maandalizi ya Kuja Mara ya Pili kwa Yesu. Ujumbe huu unaweza kufupishwa kama ifuatavyo: 1) Mungu ni Mwumbaji wako, Unapendwa na ana shauku na wewe. Ikubali karama ya neema yake na utakuwa salama katika hukumu. Mtumainie Mungu peke yake. 2)Ulimwengu huu pamoja na mifumo yake yote inayompinga Mungu, umeharibika, hauaminiki, na umeanguka. 3) Shetani, mwasisi wa mauti yote, shida, ubinafsi, na maumivu, dhambi, na wote wanaoukumbatia uongo wake, wataangamizwa upesi ili haki na upendo uweze kurejeshwa ulimwenguni. Wale tu wanaoweka matumaini yao kwa Mwokozi mwenye upendo Yesu Kristo wataokolewa milele na kubadilishwa kuwa watu wapya wanaoakisi upendo wa Mungu usio na ubinafsi.

Je! Ni shauku yako kufanya yote yaliyo katika uwezo wako ili kuufikia, kwa upendo wa Mungu, ujumbe wa toba, wokovu na hukumu, ulimwengu uliopotea? Je! utaangaza katika giza la ulimwengu, kama mwakilishi wa Kristo? Je! Utasimama, kuishi, kuongea, kujali, kubariki, na kupenda huku ukiukimbatia utambulisho wa kiunabii kama Mwadventista wa Sabato? Na kama wewe sio Mwadventista wa Sabato, Je! Ni shauku yako kujiunga na vuguvungu la Mungu la siku za mwisho, ubatizwe na kujiunga katika utume wa yesu?

**USHUHUDA WA SIFA**

- J.S.: Mungu amekuwa akifanya miujiza katika kujibu maombi yetu. Watu wamefunguliwa dhidi ya mapepo na uchawi na wengi wameponywa dhidi ya magonjwa ya kimwili.
- Viviana H.: Tumsifu Mungu kwani katika Siku 100 za Maombi, alituwezesha kuanzisha kikundi kidogo nyumbani mwetu pamoja na majirazi zetu na wameanza kumjua Yesu.
- Chadwick A.: Mtoto wangu mchanga wa kiume, ilikuwa kidogo afe kwa kupaliwa. Mapigo yake ya moyo yalipotea na hakuweza kupumua kwa muda fufani. Wote tulifadhaika na tukijaribu kufikiria chakufanya. Kisha nilikumbuka somo la Siku 100 za

Maombi la siku ile (Mtazame Yesu), na nikaomba, nikisihi kwa ajili ya uhai wake. Mungu alinipatia uthibitifu mtulivu kwamba hatakufa. Tuliweza kufanya kipimo cha CRP na baada ya dakika 15, kukiwa hakuna alama ya uhai ndani yake, alianza kupumua. Hatimaye tulimpeleka hospitalini ambako hali yake iliimarika. Sifa kwa Mungu kwa kumwokoa!

- T.E.: Nilibarikiwa mno katika Siku 100 za Maombi. Nilikuwa namwombea kaka yangu aliyekuwa amemwacha Mungu na familia yake kwa miaka 7. Hakuhudhuria hata harusi yangu. Kwa muujiza, kaka yangu alirejea nyumbani ndani ya Siku 100 za Maombi. Aliungama dhambi zake na sasa amejitoa kikamilifu kwa kazi ya Mungu!
- Orusoso A.: Katika Siku 100 za Maombi, mimi na mume wangu tumekuwa tukimwomba Mungu aiguse mioyo yetu, familia na marafiki kwenda kuwasaidia watu wakati wa zahama hii. Ingawa biashara yangu imeyumba kifedha tangu mazuio yalipotangazwa mwezi Machi, tuliwafikia watu wengi kadiri tulivyoongozwa, kwa nyakati mbali mbali ndani ya hiki kipindi. Mwanzoni mwa juma hili, nilipata msukumo wa kupitia upya fedha zangu, ndipo nilipogundua kuwa, licha ya matumizi yote kwa ajili ya matengenezo, bili na misaada kwa wengine, fedha zangu hazikuathirika kwa namna hasi kama nilivyohofia. Sifa zimwendee Mungu!

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Mwombe** Mungu akusaidie wewe na familia yako kuukumbatia utambulisho wa kiunabii, wa kitume, wa Kiadventista wa Ufunuo 14.
- **Ombea** moyo wa hiari wa kwenda kwenye shamba la utume, iwe eneo mahalia au katika nchi za kigeni.
- **Ombea** wale ambao bado wanateseka kutokana na kirusi cha corona. Ombea uponyaji na mwisho wa hili janga.
- **Ombea** kliniki inayotembea kule San Francisco ambayo huwekwa kwenye majengo ya kanisa na hutoa huduma bure za meno na macho, na kupima afya bure. Tafadhali mwombe Mungu awabariki wagonjwa kwa baraka za kimwili na uponyaji wa kiroho.
- **Ombea** watu walioghairi uamuzi wao wa kubatizwa. Omba kwamba wamkubali na kumpenda Yesu, kisha wafanye uamuzi kamili wa kujisalimisha kwake.

**Siku ya 100, Jumamosi, Julai 04, 2020**

**NITAKWENDA … HADI MWISHO**

*"*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi*."*– Mdo. 1:8

*"*Akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari*."* – Mathayo 28:18-20

*"Sisi pia tumepewa utume. Tumeamriwa kwenda kama wajumbe wa Kristo, kufundisha, kuelekeza, na kushawishi wanaume na wanawake, kuwahimiza waligeukie neno la uzima. Na kwetu umetolewa pia uhakikisho wa uwepo wa Kristo kukaa kwetu. Ugumu wo wote tunaoweza kushindana nao, majaribu yo yote tunayoweza kuyavumilia, ile ahadi yenye neema ni yetu daima, 'Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifunwa dahari.'"*– Evangelism, p. 15

**MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI**

Yesu amewaita watu wake kupeleka ujumbe wa injili hadi mwisho wa dunia, hadi mwisho wa ulimwengu juu ya kuja kwake upesi mara ya pili. Tunapoingia kuifanya kazi hii hatuna kitu cho chote cha kuogopa. Mamlaka yote ni yake! Roho wake yupo pamoja nasi ili kutuongoza na kututia nguvu! Ni jambo la ajabu kiasi gani kuwa na Yesu, Mmishonari Mkuu wa Ulimwengu, pamoja nasi . . . hadi mwisho, na zaidi ya hapo!

Kwa vile umepitia hizi Siku 100 za Maombi, kwa vile wewe na familia yako mmepitia uamsho binafsi, hebu huu moto kwa ajili ya Mungu usizimwe, bali mwingie kwa bidii katika kazi ya umishonari usio na ubinafsi, uliodhamiriwa, na wenye upendo. Jambo halitawapatia ninyi uamsho endelevu tu, bali litapelekea roho kuokolewa kwa ajili ya Yesu, na maisha ya kuridhika!

Maranatha! Je! Ni shauku yako kuchukua hii hatua ya pili pamoja na Yesu na kwa ajili yake? Kutoa maisha yote kwa utume wa huduma kwa ajili yake, po pote ulipo, na po pote akuitapo? Je! Unaitumainia neema yake kuwa yatosha kwa ajili ya changamoto zote zilizo mbele? Je! Utachagua leo kuwa zaidi ya mhudhuriaji kanisani, bali kuwa mwendaji ulimwenguni; mtu aendaye ulimwenguni kuzifikia roho pamoja na Yesu? Mungu na akubariki unaposonga mbele pamoja naye, hadi mwisho wa ulimwengu, hadi mwisho wa dahari! Maranatha!

**USHUHUDA WA SIFA**

- Sheri A.: Tulianza kufungua makanisa katika eneo la Osaka, Japani. Baada ya mwaka mmoja, bado tulikuwa hatuna mtu hata mmoja anayehudhuria ibada au kujifunza Biblia. Tuliamua kujiunga na Siku 100 za Maombi, na mahsusi kufunga na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu mwezi Mei. Ghafla, katika duka moja kubwa, Bwana akatugonganisha

na mume na mke waliokuwa waliokuwa katika kutafuta kanisa, na kumtafuta Mungu. Mara wakahitaji kujifunza Biblia. Kwa sababu ya janga hili, walikuwa hawafanyi kazi, kwa hiyo tulijifunza Biblia kila siku, na walihudhuria huduma za ibada. Mmoja wa majirani zetu pia alianza kuja kanisani. Kwa hiyo, siku ya Sabato, idadi yetu ilikuwa mara dufu, na kanisa dogo linachipua! Sifa kwa Mungu!

- N. S.: Kama sehemu ya Siku 100 za Maombi, niliahidi kuombea eneo langu kila asubuhi. Mungu alifungua mlango ambapo nilitoa masomo ya Biblia kwa wanandoa vijana. Wapo tayari kubatizwa mara masharti yatakapoondolewa! Nilipokuwa naendelea kutoa masomo ya Biblia kwa wenzi hawa, mwanamke mwingine aliyeolewa kwa mfanya biashara wa Kiislamu aliomba masomo ya Biblia kwa ajili yake na kijana wake wa kiume wa miaka 18. Kisha alimwalika binamu yake wa kike, naye akaamua kujiunga. Leo yupo tayari kubatizwa kwa sababu ya ukweli unaobadilisha maisha aliousikia. Mungu anatenda kazi!
- Unioni Misheni ya Magharibi mwa Congo: Tangu mwanzoni mwa mpango wa TMI, tulipata ugumu wa kuanzisha vikundi vidogo katika mitaa kadhaa ya Kinshasa. Baada ya janga kuanza, ililazimu kufunga makanisa makubwa na kuruhusu kuanzishwa kwa makanisa ya familia. Hadi leo, tunayo zaidi ya makanisa 200 ya familia. Hata katika maeneo ya ujirani yaliyokuwa hayana Waadventista. Makanisa haya yanashiriki uinjilisti na yameleta roho 82 kwa Bwana. Siku 100 za Maombi zimeimarisha uhusiano na ukuaji wa kiroho katika haya makanisa.

- Viviana H.: Bwana asifiwe, kwani katika hizi Siku 100 za Maombi, alituwezesha kuanzisha kikundi kidogo nyumbani pamoja na jirani zetu na wameanza kumfahamu Yesu. Kupitia ADRA tumekuwa tayari kuendelea kusaidia wakimbizi kutoka Venezuela waliopo Colombia kwa kutoa huduma za afya.
- Mungu apewe sifa kwa ajili ya mamia kwa mamia ya ushuhuda wa sifa tulioupokea! Mungu, kwa hakika, ameligeuza hili janga kuwa baraka duniani kote, watu wake walipojinyenyekesha na kuomba!

**MAMBO YA KUOMBEA**

- **Omba** kwa ajili ya uamsho endelevu kupitia kazi ya umishonari ifanyikayo kwa uaminifu hadi mwishi wa wakati. Omba kwa ajili ya kumwagwa kwa mvua ya vuli na mvua ya masika ili kazi iweze kumalizika.
- **Ombea** kazi ya utume wa kanisa katika mstari wa mbele na maeneo magumu kuyafikia ulimwenguni kote, kama vile katika dirisha la 10/40, Korea ya Kaskazini, Mashariki ya Kati, na kadhalika.
- **Omba** kwa ajili ya mahitaji ambayo hayakusemwa na hayakutajwa ambayo yamepelekwa kwa Bwana
- **Ombea** kurudi kwa Yesu upesi!

## SIKU 100 ZA MAOMBI ZIMEKWISHA, . . . KIFUATACHO NI NINI?

Tunawashukuru kwa ajili ya ushiriki wenu katika Siku 100 za Maombi pamoja na makumi ya maelfu ya kaka na dada zenu ulimwenguni kote! Asante kwa kuomba, kwa kutoruhusu hili janga liwaangushe, bali kwa kuyaweka matumaini yenu kwa Yesu na hata kuingia kazini katika kuwafikia wengine na kuwa baraka kwao katika wakati huu usio wa kawaida. Tunamshukuru Mungu kwa mamia ya ushuhuda wa sifa tulioupokea! Lakini, pia tunataka kuwatia moyo, kwamba kama bado hamjapata majibu kwa baadhi ya mahitaji, msikate tamaa. Vumilieni na iweni na imani! Mungu atayapitia katika njia yake iliyo bora, na kwa wakati unaofaa. Umilele utafunua matokeo kamili ya kile kilichofanikishwa na kinachoendelea kufanikishwa na maombi yenu endelevu kwa neema ya Mungu!

Mpango wa Siku 100 za Maombi unaweza kuwa umekwisha, lakini maombi hayajaisha! Uamsho na Matengenezo kutoka kwa Mungu upo daima! Yesu alitwambia tuendelee kumwomba **Roho Mtakatifu** (Luka 11:13); **Maombi** ni pumzi ya roho (Prayer, uk. 12); Yesu na Neno lake ni pumzi ya uhai (Yohana 6:35); Na kuna watu wengi wanaotuzunguka tunaoweza **kuwashuhudia**! Ili kukua katika kufanana na Kristo, inatupasa kujihusisha na vipengele hivi vyote muhimu vya maisha ya kiroho.
Sisi, kama timu ya *Uamsho na Matengenezo*, tunataka kukusaidia katika safari! Hapa kuna matukio machache na masomo ambayo ni ya bure kabisa, ambayo unaweza kuyafikia na kujiandikisha leo:

- **Maombi ya Pamoja** (Kwa Kiingereza)
  - Huu ni mwendelezo wa Siku 100 za Maombi. Kwa juma mara moja, utapokea wazo lenye nguvu la ibada, mahitaji ya kuombea toka kanisa la ulimwengu, shuhuda za sifa, na nyenzo mpya toka tuvuti ya Uamsho na Matengenezao
  - **Ingia:** https://www.revivalandreformation.org/signup
- **Waamini Manabii Wake** (Kiingereza, Kifaransa na Kihispania)
  - Kusoma biblia nzima na Roho ya Unabii pamoja kaka na dada zetu ulimwenguni kote. Utapokea sura moja yya Biblia kila siku, na sura moja ya Roho ya Unabii kila juma.
  - **Ingia:** https://www.revivalandreformation.org/signup
- **Kesha la EG White la kila Siku**
  - Pokea kesha la kila siku lenye wazo fupi kutoka Maandishi ya EG White.
  - **Ingia:**https://www.revivalandreformation.org/signup
- **Siku za Kuomba na Kufunga kwa Kanisa zima la ulimwengu**
  - *Julai 4, Oktoba 3, 2020*
  - *Januari 2, Aprili 3, Julai 3, Oktoba 2, 2021*
  - Kutafuta nyenzo na masomo (Kwa lugha nyingi) **Ingia:**https://www.revivalandreformation.org/prayerdays
- **Uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Kanisa (2020-2025) uitwao, "Nitakwenda"**
  - *Julai 3-4, 2020*
  - Kwa taarifa zaidi ingia: http://iwillgo2020.org
- **Siku 10 za Maombi 2021**
  - *Januari 6-16, 2021*
  - **Ingia** na upokee nyenzo zote (Kwa lugha mbali mbali) https://www.tendaysofprayer.org
- **Maktaba Inayokua ya Nyenzo za Kiroho**
  - Ingia katika Maktaba inayokua ili upate bure nyenzo za kiroho katika Maombi, Kujifunza Biblia, Kushuhudia, kushinda dhambi na changamoto, uponyaji wa kiroho, ibada na kadhalika
  - **Ingia:** https://www.revivalandreformation.org/resources
- **Tufuatilie katika Mitandao ya Kijamii:**
  - Facebook: https://www.facebook.com/revivalandreformation
  - Twitter: https://twitter.com/Revive_Reform
  - Instagram: http://instagram.com/revive_reform/